WIZARA YA ARDHI NYUMBA
NA MAENDELEO YA MAKAZI

# ARDHI BULLETIN

JARIDA LA MTANDAONI




**BODI YA UHARIRI**

**Mwenyekiti**
Eng. Anthony Sanga

**Wajumbe**
Eleuteri Mangi
Munir Shemweta
Magreth Harrison
Goodluck Mwihava
Joel Magesa
Lusajo Mwakabuku


# UZINDUZI

WA SERA YA TAIFA YA ARDHI
**YA MWAKA 1995**
TOLEO LA
**MWAKA 2023**

- Toleo Maalum - Toleo Maalum

*Issue no: 001*

# Rais Samia asisitiza mambo Sita Sekta ya Ardhi



*Mhe. Dkt.SamiaSuluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizungumza na wananchi kabla ya kuzindua Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la Mwaka 2023, Machi 17,2025 katika ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema, Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 toleo la mwaka 2023 imezingatia mambo sita muhimu yenye lengo la kuimarisha usimamizi wa sekta ya ardhi nchini.

Akihutubia wakati wa hafla ya uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 Toleo la Mwaka 2023 tarehe 17 Machi 2025 jijini Dodoma, Mhe Dkt Samia ameyataja mambo hayo kuwa ni Uimarishaji Mipaka ya Kimataifa na nchi jirani ili kurahisisha utambuzi wa alama za mipaka.

Kwa mujibu wa Mhe. Dkt. Samia uimarishaji huo wa mipaka ya kimataifa umewekwa ili kutoa nguvu katika utendaji, kutunga sheria pamoja na kuweka utaratibu wa kusimamia rasilimali zilizopo katika maji.

"Diplomasia ya kutosha ni lazima itumike ili kuelewana na majirani zetu tuweze kupima na tujue Tanzania tunakwenda mpaka wapi ili tuviepushe vizazi vyetu vijavyo na migogoro ya ardhi na mipaka huko baadaye" amesema Rais Dkt. Samia.

Jambo la pili, **kuongeza kasi ya usajili**

> **"Mambo ya msingi ya kisera yamezingatiwa ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi kwenye sekta ya ardhi" Rais Samia.**



*Mhe. Dkt.SamiaSuluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akibonyeza kitufe kuzindua Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la Mwaka 2023, Machi 17,2025 jijini Dodoma.*

**wa ardhi** ambapo katika upimaji takwimu zinaonesha takiban asilimia 75 ya ardhi nchini bado haijasajiliwa.

“Sasa tunataka kila kipande cha ardhi ndani ya nchi hii, kipangwe, kipimwe na kisajiliwe, tumerahisisha upangaji, upimaji na umilikisahaji wa ardhi ili wananchi kumiliki ardhi” amesema Rais Dkt. Samia.

Jambo la tatu, **kuimarisha uwezo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini** kwa kuanzishwa Mabaraza ya Ardhi katika ngazi kijiji, kata na wilaya. Katika Sera hii mfumo wa Mabaraza ya Ardhi inapitiwa upya ili kuimarisha mifumo ya udhibiti wa vyanzo vya migogoro ya ardhi kwa kutumia TEHAMA.

Jambo la nne, **kuimarisha uthamini na ulipaji wa fidia** kwa haki, kwa wakati na thamani halisi na kuwahimiza watumishi wanaoratibu suala la fidia wabadilike, waende kufanya kazi kwa weledi na kusimamia haki ili wananchi wapate fidia kwa wakati na viwango sahihi.

Jambo la tano, **kuimarisha uwekezaji** katika uendelezaji wa ardhi ambapo Sera hii inavutia uwekezaji na imeweka utaratibu wa waendelezaji milki (Real Estate) wa kigeni kuwekeza katika nyumba na kuuza kwa wenye uhitaji na kusisitiza nyumba ziende juu ili ardhi itumike vizuri zaidi.

Jambo la sita, **kuimarisha utunzaji wa taarifa kwenye sekta ya ardhi,** hatua hii inasaidia kuimarisha utendaji kazi na kuondoa mianya ya kukwamisha na kuchelewesha utoaji huduma kwa wananchi.

Ndiyo maana Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inahimiza kuwa Sera ya Ardhi ni Msingi wa Ustawi na Maendeleo Endelevu ya Taifa, “Kazi Iendelee.”

> **“watumishi wanaoratibu suala la fidia wabadilike, waende kufanya kazi kwa weledi na kusimamia haki” Rais Samia.**



# SERA YA ARDHI ILIYOBORESHWA KUWEKA MFUMO MADHUBUTI MATUMIZI YA ARDHI

Na Mwandishi wetu



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema kuwa Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la Mwaka 2023 iliyozinduliwa Machi 17, 2025 jijini Dodoma ina lengo la kuhakikisha nchi inakuwa na mfumo madhubuti na wenye usawa wa umiliki, upatikanaji na usimamizi wa matumizi ya ardhi kwa maendeleo endelevu.

Rais Samia amesema hayo wakati akizindua Sera ambapo pamoja na mambo mengine, amewahakikishia Watanzania kuwa misingi iliyowekwa kwenye Sera hiyo ya mwaka 1995 toleo la mwaka 2023 haijabadilishwa bali inaboresha utoaji huduma ya Sekta ya Ardhi nchini.

"Ardhi itaendelea kuwa mali ya umma na Rais ndiyo mdhamini kwa niaba ya wananchi wote, haki ya kumiliki na kutumia ardhi iliyopatikana ama kwa kumilikishwa au serikali au kimila itaendelea kuwa mifumo pekee ya kumiliki ardhi, tulichokiondoa ni mila potofu ya kwamba mwanamke hawezi kumiliki ardhi" amesema Rais Samia.

Ameyataja masuala sita yaliyopo katika sera hiyo ikiwemo kuyajumuisha na kuyapa msingi wa kisera masuala muhimu ambayo hayakuzingatiwa kwenye sera iliyopita ikiwemo zoezi la uimarishaji mipaka ya kimataifa ya Tanzania na nchi jirani, kubainisha haja ya kuweka utaratibu wa kisera wa kusimamia uchumi wa rasilimali zilizopo kwenye maji kwa kupima na kumilikisha ardhi hizo pamoja na kujumuisha lengo la kuimarisha usimamizi wa soko la ardhi nchini.

## UTHAMINI

Sera itaimarisha uthamini na ulipaji wa fidia, itaimarisha uwekezaji katika uendelezaji wa ardhi na kusaidia katika kukabili migogoro ya ardhi kwa kutumia TEHAMA pamoja na kuzingatia hoja za muda mrefu za Diaspora wa Tanzania kuhusu kuwa na haki ya kutumia ardhi yao ya Tanzania.



*Waziri wa Ardhi, Mhe. Deogratius Ndejembi akitoa maelezo ya awali kabla ya Rais kuhutubia.*

## WIZARA YAPONGEZWA

Rais ameipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wataalam na wadau walioshiriki kufanikisha kuandaliwa kwa sera hiyo pamoja na mabadiliko makubwa yaliyofanyika chini ya wizara hiyo kutoka kuwa Wizara ya migogoro, uzembe wa makusudi hadi kuwa Wizara ya maendeleo ya watu.

## SERA YA KISASA

Waziri wa Ardhi amesema Sera hiyo inaendana na hali halisi na nyakati za sasa ambapo imezingatia kando mila na desturi zilizopitwa na wakati katika masuala ya ardhi.

"Pamoja na hayo, tunashukuru kwa fedha zaidi ya dola za Marekani milioni 65 za kutengeneza upya ramani za msingi katika nchi yetu ambapo ikifika mwaka 2030, Wizara itakuwa imetekeleza agizo lako la kupima nchi yote na kuipanga kulingana na mahitaji ya eneo husika"



*Rais Samia akimkabidhi mfano wa funguo ya gari Waziri wa Ardhi Mhe. Deogratius Ndejembi alipomkabidhi magari 70.*



*Rais Samia akikagua moja ya magari 70 aliyoyakabidhi Wizara ya Ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za umilikishaji ardhi.*



*Sehemu ya Magari yaliyokabidhiwa kwa Wizara ya Ardhi na Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa hafla ya uzinduzi.*

# SAMIA ATAKA MABORESHO YA MAKAZI KATIKA MAJIJI NA MIJI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesistitiza umuhimu wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kufanya maboresho ya makazi kwenye majiji na miji sambamna uwepo wa nyumba za bei nafuu kwa wananchi.

Dkt. Samia ametoa mfano wa baadhi ya makazi duni yaliyopo kwenye maeneo ya jiji la Dare es salaam ikiwemo Mwananyamala na kinondoni huku akisisitiza umuhimu wa majiji na miji kuwa na hadhi na sura inayoendana na miji na majiji.

Kwa upande wake Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Deogratius Ndejembi alisema kutokana na miji kukua kwa kasi kuna kila sababu ya kuwa na mpango mahsusi wa ardhi kupangwa, kupimwa na kumilikishwa hatua itakayowezesha kutambua kila kipande cha ardhi na matumizi yake na hivyo kuondoa migogoro ya ardhi. Ameipongeza serikali ya awamu ya sita chini Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya ardhi tangu alipoingia madarakani mwaka 2021.

“Yapo mambo mengi ambayo yamekuwa yakifanyika kama vile suala la wizara kuhakikisha inapanga, inapima na kumilikisha ardhi na hapa umetoa zaidi ya shilingi bilioni 50 katika mfuko wa KKK ili kufanikisha suala hilo” alisema Mhe. Ndejembi.

Pia Waziri Ndejembi alisema Rais ametoa takriban Tsh Bilioni 135 ambapo kupitia fedha hizo wizara imepata vitendea kazi mbalimbali yakiwemo magari 70 aliyoyazindua ambayo yanaenda kutumika katika mikoa na halmashauri.

“Haya yote yamekuwa ukuyafanya wewe Mhe. Rais lakini pia umetoa dola za kimarekani milini 65 kwa ajili ya kutengeneza ramani za msingi katika nchi yetu, mara ya mwisho ilipimwa 1978 katika kutengeneza ramani ya msingi. Wewe umeona umuhimu na katika kipindi chako ukatoa fedha hizo na kuna maeneo mengi umefanya katika sekta hii ya ardhi’’ alisema Mhe, Ndejembi.




Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akipata maelezo ya utekelezaji wa Program ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) katika mikoa mbalimbali kutoka kwa Waziri wa Ardhi Mhe. Deogratius Ndejembi wakati wa uzinduzi wa Sera ya Taifa a Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la Mwaka 2023 jijini Dodoma.





Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amemuagiza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo Mhe Deogratius Ndejembi kuwachukulia hatua watendaji wanaolalamikiwa na wananchi katika Wizara ya Ardhi.

# "Watumishi Vikwazo wa Sekta ya Ardhi Wachukuliwe Hatua Za Kinidhamu" - Rais Samia

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amemuagiza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo Mhe Deogratius Ndejembi kuwachukulia hatua watendaji wa sekta ya ardhi ambao ni kikwazo na sababu ya malalamiko ya wananchi na wanakwamisha ustawi wananchi katika sekta ya ardhi.

Ametoa maagizo hayo wakati wa uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la Mwaka 2023 ambayo pamoja na mengine kila mmiliki wa ardhi atatambuliwa na milki yake kusajiliwa hatua itakayosaidia kushughulikia changamoto za sekta ya ardhi.

Alisema, mtendaji yoyote wa sekta ya ardhi atakayekwamisha utekelezaji wa masuala ya ardhi anapaswa kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwani matarajio ya wananchi ni makubwa kwa serikali yao kupitia Sera ya Ardhi.

Aidha, Rais Samia ametaka kuimaraishwa kwa upimaji, usajili na usimamizi wa ardhi huku akiitaka wizara ya Ardhi kupitia upya mfumo wake wa kitendaji kwa kuangazia umuhimu wa kuwa na Kamisheni ya Ardhi itakayokuwa na majukumu ya usimamizi wa ardhi nchini katika dirisha moja la kuhudumia wananchi.

**"Mtendaji yoyote wa sekta ya ardhi atakayekwamisha utekelezaji wa masuala ya ardhi anapaswa kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwani matarajio ya wananchi ni makubwa kwa serikali yao kupitia Sera ya Ardhi" Rais Samia.**



Sehemu ya viongozi na wananchi waliohudhuria uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la mwaka 2023 uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete Machi 17,2025 jijini Dodoma

# RAIS SAMIA AZINDUA MFUMO WA KIDIJITI e-ARDHI




*Mhe. Dkt.SamiaSuluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akibonyeza kitufe kuzindua rasmi mfumo wa kidijiti unaokwenda kutatua changamoto katika sekta ya ardhi nchini Machi 17, 2025 katika ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.*

Na Mwandishi Wetu

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan amezindua rasmi mfumo wa kidijiti unaokwenda kutatua changamoto katika sekta ya ardhi nchini.

Rais amezindua mfumo huo wa e- Ardhi utakaowezesha Hati Miliki za Ardhi kutolewa kidijiti ndani ya muda mfupi na hivyo kuondoa changamoto ya kiwanja kimoja kumilikishwa kwa watu wawili.

Akielezea mfumo unavyofanya kazi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Deogratius Ndejembi anasema, awali hati milki za ardhi zilihifadhiwa kwenye mfumo wa makaratasi na hivyo kujaza ofisi za masijala.

“Kuna wakati karatasi hizo zilikuwa zinapotea na kuleta migogoro ya kupewa hati mara mbili, lakini mfumo wa e-Ardhi utalikomesha hilo na mfumo huu unasomana na mifumo ya taasisi nyingine ya serikali ikiwemo Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Amesema, mfumo huo umeanza kutumika katika Salaam, na Dodoma na uko katika hatua za mwisho kukamilika kuanza kutumika katika mkoa wa Mbeya.

Ndejembi anasema hadi kufikia 2027 watakuwa wamekamilisha mfumo huo utakuwa unatumika nchi nzima na kuhakikisha nyaraka zote zinaingia katika mfumo huo zinachukua




*Mhe. Dkt.SamiaSuluhu Hassan akimkabidhi Hati Milki ya Ardhi ya Kieletroniki Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi Mhandisi Anthony Sanga mara baada ya kuzindua Mfumo wa e-Ardhi wakati wa uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 toleo la mwaka 2023 jijini Dodoma.*

# Uzinduzi wa Sera Ya Ardhi ni Tukio la Kihistoria- Zungu



Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Musa Azan Zungu amesema tukio la Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 toleo la Mwaka 2023 hilo ni la kihistoria kutokana na kusubiriwa kwa kubwa wake.

"Mhe. Rais, tukio hili ni muhimu na la kihistoria kwetu kwani kwa kipindi kifupi cha uongozi wako mambo mengi yaliyosubiriwa sasa unayaleta na kuhakikisha taifa linaendelea kuwa na amani na migogoro hii ya ardhi kama ile ya wakulima na wafugaji inasimamiwa katika sera hii" alisema Mhe. Zungu.

Katika salamu zake kwa niaba ya Mhe. Tulia Akson, Spika wa Bunge anayehudhuria mkutano wa Mabunge, Naibu Spika amesema, kulikuwa na changamoto mbalimbali kwenye sera ya ardhi lakini sasa ni wakati mzuri wa kutatua changamoto hizo hususan migogoro ambayo wananchi wetu wanakumbana nayo.

"Niwaombe watendaji, ardhi ni rasilimali kubwa sana tusikalie uchumi, tuifanye ardhi iwe na mchango mkubwa kwenye pato kuu la serikali" Alisema Mhe. Zungu.

# WIZARA YA ARDHI BARA NA ZANZIBAR KUENDELEA KUSHIRIKIANA – MHE. SALHA

Na Mwandishi Wetu

Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma amesema, wizara yake itaendelea kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Tanzania Bara) katika kuhakikisha kuwa maono ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais Dkt. Hussein Mwinyi yanafanikiwa katika kurasimisha ardhi na kuleta tija ya ardhi na makazi kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Akizungumza wakati wa Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la Mwaka 2023, Mhe. Salha amesema, kuwepo kwa mashirikiano makubwa kati ya wizara hizi mbili yamesaidia Zanzibar kuandaa Sera mpya ya Ardhi itakayoenda kukabiliana na changamoto mbalimbali za sekta ya ardhi visiwani Zanzibar.

Mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Salha ameeleza hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuboresha sekta ya ardhi, akisema Serikali ya Zanzibar ipo kwenye mchakato wa kufuta Mahakama ya Ardhi na badala yake watakuja na Mabaraza ya Ardhi, suala ambalo kwa sasa linajadiliwa na Baraza la Mapinduzi visiwani humo.

Aidha, Mhe. Salha amesema Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar imezindua mpango mkakati wenye sera na mfumo wa kielektroniki utakaosaidia kupanga matumizi ya ardhi visiwani humo kama sehemu ya kuongeza thamani ya ardhi.



*Naibu Waziri wa Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma akizungumza wakati wa uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la Mwaka 2023 jijini Dodoma.*

# BURUDANI YANOGESHA UZINDUZI WA SERA YA TAIFA YA ARDHI



Hafla ya uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la Mwaka 2023 ulipambwa kwa shamrashamra na burudani mbalimbali kutoka vikundi vya ngoma na wasanii ambazo zimenogesha hafla hiyo iliyofanyika jijini Dodoma ambapo Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiye alikuwa Mgeni Rasmi.

Vikundi vya burudani vilivyotumbuiza katika hafla hiyo na kukonga nyoyo za wananchi waliohudhuria hafla hiyo ni kikundi cha Ngoma cha Mchoya kutoka Dodoma kilichocheza ngoma iliyoambatana na wimbo unaoelezea sera sambamba na ngoma ya Kibati kutoka Zanzibar.



Kwa upande wa Wasanii, Mrisho Mpoto alitumbuiza kwa igizo lililoambatana na wimbo ambapo lilivuta hisia na kuwahuzunisha wengi kutokana na namna lilivyoelezea jinsi mwanamke anavyonyanyaswa katika suala la mirathi.




Aidha, wasanii wawili kutoka mkoa wa Njombe ambao ni Masai the Don na Mac Ford walitoa burudani ya aina yake na kuzikonga nyoyo za wananchi waliohudhuria hafla hiyo. Vile vile wana utenzi kutoka Zanzibar nao walikuwa sehemu ya wasanii waliotoa elimu kwa njia ya utenzi maridhawa kuhusiana na Sera ya Taifa ya Ardhi na kuburudisha hadhira iliyofurika ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma takriban wageni zaidi ya 3400 kwenye hafla hiyo.

# Matukio katika Picha



*Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akipata maelezo mbalimbali kutoka kwa Waziri wa Ardhi Mhe. Deogratius Ndejembi wakati wa uzinduzi wa Sera ya Taifa a Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la Mwaka 2023 jijini Dodoma.*



*Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Rosemary Senyamule akitoa salaam za Mkoa wakati wa uzinduzi jijini Dodoma.*



*Msanii Masai the Don akitumbuiza mbele ya wageni waalikwa wakati wa uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi*

*Sehemu ya viongozi na wananchi waliohudhuria uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la mwaka 2023*





*Rais Samia akimkabidhi mfano wa funguo ya gari Waziri wa Ardhi Mhe. Deogratius Ndejembi alipokabidhi magari 70*

*Kikundi cha Ngoma cha Mchoya kutoka Dodoma kikitumbuiza wakati wa hafla ya Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi jijini Dodoma*





*Sehemu ya umati uliojitokeza kwa wingi kushiriki uzinduzi wa Sera ya Ardhi jijini Dodoma*